

# OFISI YA RAISI – TAMISEMI HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO



SHULE YA SEKONDARI KITOWO,  
S. L. P 2313,  
**KILOLO**  
Tarehe: .....

JINA LA MWANAFUNZI: .....  
SHULE ANAYOTOKA:.....

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KITOWO WILAYA YA KILOLO MKOA WA IRINGA KWA MWAKA 2021

### 1.0UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza (I)** katika shule hii mwaka **2021** Shule ya sekondari Kitowo ipo umbali wa **km 22** Kaskazini/Mashariki/ Magharibi/ kusini mwa mji mkuu wa mkoa/halmashauri ya Wilaya ya **KILOLO**. Usafiri wa kutoka mjini **IRINGA** unapatikana katika kituo cha mabasi cha **MLANDEGE** kwa nauli ya **Tsh 3,500/=**. Mhula wa kwanza wa masomo unaanza **Tarehe 11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **Tarehe 06/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni **Tarehe 18/01/2021**.(Atakaye chelewa kumleta mwanafunzi hatua Kali itachukuliwa dhidi yake)

### 2.0SARE ZA SHULE

#### (a) WAVULANA

- (i) Suruali 2 za rangi ya **DAMU YA MZEE**. Mshono: chini upana **inchi 18 yenye mkunjo, marinda** 2 juu ya mifuko ya mbelena mfuko wa nyuma usiwe na zipu. Mkanda wa suruali upana wa **inchi 2** wenye luksi (Zingatia rangi ya kitambaa kilichoambatanishwa).
- (ii) Mashati mawili (2) **meupe** (tetron) mikono **MIFUPI**.
- (iii) Viatu jozi mbili (2) vya **ngozi, vyeusi** vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
- (iv) Soksi jozi mbili (2) au zaidi rangi **NYEUSI**
- (v) Sweta rangi ya **BLUU** yenye **(V)** upande wa mbele isiyo na maandishi/mchoro
- (vi) Mkanda **mweusi** usiwe na nembo yoyote.
- (vii) Sare za michezo raba na trakisuti rangi ya **BLUU BAHARI**, T.shirt rangi ya **BLUU au NYEUSI** na raba.

## **(b) WASICHANA**

- (i) Sketi mbili (2) ndefu **INAYOGUSA VIATU** rangi ya **DAMU YA MZEE**. Mshono: **RINDA BOX** yenye mfuko upande wa kushoto, mkanda inchi 2. (Zingatia rangi ya kitambaa kilichoambatanishwa).
- (ii) Shati (blauzi) mbili nyeupe (tetron) mikono **MIFUPI**.
- (iii) Viatu jozi mbili (2) vya ngozi, vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
- (iv) Soksi jozi mbili (2) au zaidi rangi **NYEUPE**
- (v) Sweta rangi ya **BLUU** yenye **(V)** upande wa mbele isiyo na maandishi/mchoro
- (vi) Hijabu **(NYEUPE)**.
- (vii) Sare za michezo raba na trakisuti rangi ya **BLUU BAHARI**, T.shirt rangi ya **BLUU au NYEUSI** na raba.

## **3.0 VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

- (i) Daftari **18 (COUNTER BOOK QUIRE 3 ZIWE 9 NA DAFTARI ZA MSOMI ZIWE 9)**.
- (ii) Kalamu **10** na penseli **4**
- (iii) Mkebe **1** wa hesabu na **school ruler (cm 30) 1**
- (iv) Begi la kubebea daftari
- (v) Kamusi **1** ya kiingereza (DICTIONARY)
- (vi) Rimu bunda **1** (A4)
- (vii) **JALADA 1** (box file) la kutunzia kumbukumbu zake

## **4.0 MAHITAJI YA KIBINADAMU**

### **(i) MATIBABU**

Mwanafunzi aje na kadi ya CHF (Kadi ya bima ya Afya) kwa ajili ya matibabu. **(Jukumu la Matibabu ni la Mzazi/Mlezi)**

### **(ii) CHAKULA**

Kila mwanafunzi atachangia chakula cha mchana kwa wale wa kutwa na wale wa hostel kwa milo yote mitatu akiwa shuleni. **(Jukumu la Chakula ni la Mzazi/Mlezi)**

### **(iii) VIFAA VYA USAFI KWA WOTE**

AJE NA VIFAA VIFUATAVYO;

- (a) Fagio ya chelewa moja **(1)**
- (b) Ndoo (wasichana **2**, wavulana **1**) ujazo wa **lita 10**
- (c) Jembe lenye mpini **1**
- (d) Fyekeo/Kwanja **1**

**N.B Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na nakala ya cheti cha kuzaliwa.**

## **5.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri kwa kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
- (d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo kikamilifu juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- (i) Kutunza mali za umma.

**5.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:**

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumzi ya madawa ya kulenya kama vile uvutaji Bangi, Cocaine, Mirungi na Kubeli.
- (e) Kupigana au kupiga.
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- (h) Kuwa mjamzito/kupata Mimba.
- (i) Kuoja au kuolewa.
- (j) Kutoa mimba.
- (k) Kugoma, Kuchochea na Kuongoza au Kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- (m) Kuwa na simu ya mkononi.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

SAINI .....

ADELIA PIUS MVEYANGE

**MKUU WA SHULE - 0765 940067**

# KUKUBALI NAFASI

Mimi .....  
Ninakubali/sikubali mwanangu .....  
Ajiunge na shule ya Sekondari ..... na kwamba nitampa/sitampa  
vifaa na mahitaji yatakayohitajika kama iliyoagizwa na Uongozi wa Shule.

Vile vile ninaahidi kuwa nitatoa ushirikiano wa hali ya juu kwa walimu katika kumlea  
mtoto wangu kadiri ya maadili ya mwanafunzi wa Kitanzania mpaka atakapomaliza  
kidato cha nne.

## ANUANI YANGU

.....  
.....  
.....

**SIMU NA.** .....

**SAINI** .....

Iwapo mtoto atapatwa na tatizo kubwa ghafla/kiafya au ajali, mtu mwingine wa  
karibu;

1. Jina: .....  
Kijiji: .....  
Anwani yake: .....  
Namba ya Simu: .....

2. Jina: .....  
Kijiji: .....  
Anwani yake: .....  
Namba ya Simu: .....

**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING  
KITOWO SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by a medical officer in respect all Form I entrants.

Pupil's full name: .....  
Age: .....Year: ..... Sex.....  
Blood count (Red and White): .....  
Stool examination: .....  
Syphilis and other venereal diseases test: .....  
T.B. test: .....  
Eye test: .....  
Ears: .....  
Abdomen:  
.....  
Urine for plane test: .....  
Test for Pregnancy (for girls only): .....

**ADDITIONAL INFORMATION**

(If any) e.g Physical defects impairment  
Infections chronic or family diseases etc.

.....  
.....  
.....  
.....

I certify that the above is fit/unfit to pursue his/her lessons/duties as required

Station ..... Signature: .....

Date: ..... Designation: .....

**Note: Medical Officer**

At the time of examination please treat the individual for any ailments you note, pupils/employee. This completed form should be sent to the school with your acceptance form brought when you came to school. No pupils enroll or any person employment with no certificate or physical fitness.